KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

# Jarida la SAUTI YA JIJI DAR ES SALAAM

Toleo Namba 0016- Julai 2024

# MCHENGERWA AIPONGEZA ILALA UBUNIFU WA SARE ZA BODABODA

- Aelekeza Mikoa yote kuwasajili Madereva kwenye kanzi data
- Awataka Wakurugenzi wa kuweka utaratibu wa Mikopo kwa Bodaboda







## CPA Makalla Aridhishwa na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Jiji la DSM

## BILIONI 10.75 ZATENGWA KUTENGENEZA BARABARA JIJI LA DSM





SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA MAENDELEO YA TAIFA

# Waziri Mchengerwa awataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa Walezi wa madereva wa Bodaboda na Bajaji




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa amewataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa Walezi wa madereva boda boda na bajaji Nchini, Mhe. Mchengerwa ametoa maelekezo hayo Julai 01,2024 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salam, wakati wa uzinduzi wa sare maalum (uniform) na mfumo wa kidijitali (kanzidata) wa madereva Bodaboda na Bajaji wa jiji la Dar es Salaam.

"Ninawakaka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kila mmoja wenu akawe mlezi wa madareva boda boda na bajaji kwani taifa letu linamtegemea kila mmoja wetu kushiriki ujenzi wa nchi na ndio maana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan itaendelea kuwathamini na kuwajali madereva wa boda boda na bajaji." Amesisitiza Mhe.Mchengerwa.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Mhe. Mchengerwa amempongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala pamoja na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwa ubunifu walioufanya wa kuhakikisha wanawatambua bodaboda na bajaji wa Wilaya ya Ilala kwani ubunifu huu unawaunganisha madereva hao kuweza kushirikiana katika mambo mbalimbali ya kujenga Taifa huku akitoa Wito kwa Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Nchi kwa ujumla kufanya hivyo.

Sambamba na Hilo Mhe. Mchengerwa amewataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote Nchini kuhakikisha wanawalinda na kuwajali maafisa usafirishaji (madereva bajaji na bodaboda) kwa kuwatambua katika vituo vyao vya maegesho pamoja na kuhakikisha wanajisajili kwenye mfumo wa kidijitali huku akiwataka kushirikiana na Halmashauri zao kuwajengea maafisa usafirishaji hao vituo vya maegesho ambavyo vitawasaidia kujikinga na Mvua pamoja na jua.

"Nipende kutoa pongezi kwa Wilaya ya Ilala kwa kuwaunganisha maafisa usafirishaji hawa kwani hafla hii inaonesha kuwajali na kuwathamini vijana hawa hivyo katika kutambua mchango wao ninaagiza Halmashauri zote Nchini kuhakikisha katika Mgawanyo wa asilimia 10% za mapato ya Halmashauri na maafisa usafirishaji hawa hawakosekani pia muache kukamata kamata ovyo zaidi mtumie Kamati za ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa kutoa elimu kwa vijana hawa juu ya usalama barabarani".

Halikadhalika Mhe. Mchengerwa amewataka Waganga Wakuu wa Wilaya kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa maafisa usafirishaji hao ili kuepusha ajali mbalimbali ambazo zimekua zikitokea huku akiwahimiza maafisa usafirishaji hao kuweka utaratibu wa kukutana mara kwa mara kujali mambo mbalimbali ya kuwajenga kwani Serikali ya awamu ya Sita Chini ya Rais MheShimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu na inawathamini sana.

Vilevile amewaomba wadau wa maendeleo kutumia fursa hii ya sare maalum za badaboda kutangaza biashara zao kwa kuwatengenezea maafisa usafirishaji hao sare hizo na kuwapa bure kwani kupitia sare hizo wataweza kujitangaza na ukizingati vyombo hivyo vinazunguka maeneo mengi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila amempongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwaunganisha bodaboda na bajaji hao huku akitoa wito kwa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kuwekeza zaidi kwenye kutoa elimu kwa maafisa usafirishaji hao na sio kuwakandamiza kwa ushuru wa maegesho yasiyo rasmi( Wrong Parking).

Aidha Mhe. Chalamila aliendelea kusema "Tutaona ni namna gani ya kuwasaidia madereva hawa katika kupunguza gharama za tiba kwa madereva wanaopata ajali na kupelekwa MOI ila niwatake madereva bajaji na bodaboda kuwa mabalozi nyie wenyewe kwa kujenga ustarabu katika kuendesha vyombo vya moto pamoha na kutii sheria za barabarani ili kuepukana na ajali zisizo za lazima."

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo ameeleza kuwa " Sisi kama Wilaya ya Ilala tushaanza kuwatambua bodaboda wote na tumewatengea vituo maalumu kwaajili ya maegesho kwani kuwatambua na kuwarasimisha inaleta utu na kuwajali maafisa usafirishaji hawa hivyo sisi kama Jiji la Dar es Salaam tutapokea maelekezo kwa utekelezaji na tunaahidi kuwapanga maafisa usafirishaji hawa katika maeneo maalumu lengo likiwa ni kuunga Mkono Juhudi za Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutunza mazingira na kuhakikisha usalama wa kila mwananchi hivyo sisi tutakwenda kuwalinda na kuwatetea bodaboda na bajaji kwenye changamoto zao ili kuwa sehemu ya Mafanikio ya Nchi yetu, pia tutahakikisha asilimia 10% ya mapato ya maegesho yatakwenda kwenye Saccoss yao lengo likiwa ni kuhakikisha vijana hawa wanapata maisha bora."

Vilevile Mhe. Mpogolo amewataka madereva hao kutii sheria za barabarani ili kuepuka ajali za mara kwa mara bila kusahau kuvaa sare maalumu kwani takwimu zinaonyesha katika Hospitali ya Taifa Muhimbili Kitengo cha mifupa (MOI) takribani wagonjwa 5900 ya wagonjwa wote ni ajali za bodaboda hivyo ili kuepuka ongezeko hili Wilaya ya Ilala ikaona ni vyema kuanzishwa kwa Sare maalumu na mfumo wa kidijitali kwa vijana hao hii itawatambua madereva hawa kwa uharaka zaidi na Jiji la Dar es Salam litakua linapendeza na ajali zitaepukika.

Kwa upande wake Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Kanda Maalumu ya Dar es Salaam (ZTO), Kamishna Msaidizi wa Polisi, ACP. William Mkonda amewaasa madereva boda boda kuvaa helement pamoja na kutii sheria za barabarani kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kujiepusha na ajali za mara kwa mara zisizo za lazima.

Akitoa shukrani zake kwa niaba ya maafisa usafirishaji (bodaboda/bajaji)Naibu Katibu wa Shirikisho la bodaboda na bajaji Tanzania ambaye pia ni Katibu wa bodaboda na bajaji Mkoa wa Arusha Bw. Hakim Msemo ameeleza kuwa , wao kama maafisa usafirishaji watatii sheria bila shuruti pamoja na kutekeleza yote waliyoelekezwa ikiwemo kuvalia sare maalumu na kujisajili katika mfumo wa Kidigitali(Kanzi Data) wa madereva bodaboda na bajaji kwani imami yao ni kuhakikisha vifo vya ajali za bodaboda vinapungua au kutokomea kabisa kama ilivyo kwa Nchi ya Uganda huku akiiomba Serikali kuwafungulia Sacoss kwa ajili ya kujiwekeza maafisa usafirishaji ambayo itawasaidia katika kukabiliana na changamoto za maisha.

Aidha muonekano wa Sare Maalumu yenye namba ya usajili katika kanzi data utasaidia kuthibiti vitendo vya uhalifu, kupunguza ajali za barabarani pamoja na kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali kupitia malipo ya leseni za udereva, leseni za biashara na Maegesho.



# CPA Makalla Aridhishwa na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Jiji la DSM



KATIBU wa NEC, Siasa, itikadi, Uenezi na mafunzo CCM Taifa, CPA Amos Makalla, ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi( CCM).

CPA Makalla amebainisha hayo Julai 8, 2024 Jijini Dar es Salaam, akiendelea na ziara yake katika Jimbo la Segerea ambapo alitembelea mradi wa ujenzi wa ghorofa 20 Shule ya Sekondari Minazi Mirefu wenye thamani ya shilingi bilioni 1.79 pamoja na Mradi wa Kituo cha Afya Kinyerezi chenye thamani ya shilingi milioni 500.

Akiwa kwenye ziara hiyo CPA. Makalla Ameipongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa utekelezaji mzuri wa miradi kwani thamani ya fedha inaonekana na miradi imetekelezwa kwa kiwango cha juu.

“Niwapongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Jiji kwa utekelezaji wa miradi kwani Jitihada za Serikali za kuboresha huduma kwa wananchi zinaonekana pia mmeweza kutekeleza miradi hii kwa kutumia fedha za mapato ya ndani na nyingine za Serikali kuu hizi ni jitihada nzuri mnazozifanya za kuendelea kuboresha huduma za afya na Elimu kwa Wananchi wa Jiji la Dar es Salaam.

Sambamba na hilo CPA Makalla amemshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt . Samia Suluhu Hassani kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha sekta za Elimu na Afya zinaboreshwa na huduma zinawafikia wananchi kwa Wakati huku akiwataka Waganga Wafawidhi kuhakikisha huduma zinaboreshwa kwa Wananchi kwa kuwatia moyo na kuhakikisha majengo mazuri yananendana na huduma bora.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo ameeleza kuwa “ Tunatoa Shukrani zetu kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha huduma za elimu na afya katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwani fedha nyingi zimekua zikiletwa kwaajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu lengo likiwa ni kuhakikisha sekta hizo zinakua imara na wanachi wanapata huduma bora na kwa wakati.

Aidha Mhe. Mpogolo ameendelea kusema Serikali imeendelea kuwekeza katika sekta ya elimu na Afya kwani katika Jiji la Dar es Salaam Shule za ghorofa zaidi ya 8 zinaendelea kujengwa zikiwa katika hatua mbalimbali hii itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuongeza ufaulu zaidi.



# Jiji la DSM latwaa Tuzo Maonesho ya 48 ya Sababsaba




Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na divisheni ya Maendeleo ya Jamii washiriki maoenesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya **Maonesho vya Mwl. J.K Nyerere (SabaSaba) Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam** ambapo wametwaa tuzo ya washindi wa tatu katika ngazi za Halmashauri.

Maonesho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Mwl. J.K. Nyerere
Wilayani Temeke yalianza tarehe 28 Juni, 2024 na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa ameambatana na Rais wa nchi ya Msumbiji Mhe. Filipe Nyusi na yanatarajiwa kufungwa tarehe 13 Julai, 2024.

Aidha, ushiriki wa maonesho hayo ya 48 ya Kimataifa ya biashara kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yametoa fursa kwa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Idara ya Maendeleo ya Jamii kutangaza na kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma zinazopatikana ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**"Kwetu sisi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam maonesho haya yanatupa nafasi ya kuwahudumia wananchi kwa ukaribu zaidi kwani tunatoa leseni mbalimbali pamoja na elimu kwa wanachi juu ya huduma zetu pamoja na kutangaza fursa kwa wajasiriamali za namna ya kujikwamua kupitia mikopo ya asilimi 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri."** Bussa Musika, Afisa Biashara.

Maonesho hayo ya 48 ya Kimataifa ya ya biashara kwa mwaka huu yamebeba kauli mbiu isemayo 'Tanzania mahali sahihi pa Biashara na Uwekezaji.'



# HABARI PICHA

**Viongozi mbalimbali wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam walivyotembelea bada la Jiji la Dar es Salaam kwenye Maonesho ya Sabasaba 2024 katika viwanja vya Mwl Nyerere Jijini Dar es Salaam**


















# Mkuu wa Wilaya ya Ilala Atoa Wito kwa Vijana Kuachana na Matumizi ya Dawa za Kulevya



Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo amewataka Vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya na badala yake waungane katika kufanya shughuli halali za kiuchumi ili wajiletee maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na hata Taifa.

Mheshimiwa Mpogolo ametoa wito huo Julai 05 2024, wakati wa akifunga Kongamano la Vijana la Kapinga Matumizi ya Dawa za Kulevya lililofanyika katika viwanja vya Usikate Tamaa vilivyopo Vingunguti Jijini Dar es Salaam sambamba na kauli mbiu isemayo ‘WEKEZA KWENYE KINGA NA TIBA DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA” ambayo inalenga Serikali, wadau, vijana na wananchi kwa ujumla kuwa na dhamiri ya dhati katika kuwekeza kwenye kinga na tiba ilikupunguza au kuondoa kabisa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa vijana kwani kinga na tiba, ni uhakika wa ushindi wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Akizungumza na vijana pamoja na Wananchi waliohudhuria katika Kongamano hilo Mhe. Mpogolo amesema “Kufuatia wimbi la vijana kuingia katika matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na kupata madhara mbalimbali ya kiafya Serikali imejikita katika kutoa elimu ili jamii ifahamu, hivyo Kwa juhudi zinazoendelea za kupambana na matumizi ya madawa ya kulevya, nitoe pongezi na shukrani za dhati kwa kazi kubwa inayofanywa na Uongozi wa Halmashauriya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo MDH, DEH pamoja na Peer to Peer group katika kuchochea, kuhamasisha na kuratibu shughuli zote za mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na kuwekeza kwenye kinga na tiba dhidi ya dawa za kulevya. pia niwasihi vijana wengine ambao hamjaingia kwenye madawa msishawishike kuingia huko na ambao mshaathirika na madawa muendelee kutumia dawa za kuwakinga ili msiathirike zaidi.”

Sambamba na hilo Mhe. Mpogolo amewataka Vijana kuwa na Maadili mema pomoja na kujiepusha na makundi ya ushawishi ili kulinda afya zao na nguvu kazi ya taifa huku akiwataka wajikite zaidi na Shughuli za kimaendeleo pamoja na kuwasisitiza vijana hao kuwa mabalozi wazuri katika kuwaelimisha wale wote ambao hawakupata nafasi ya kushiriki katika kongamano hilo kuhusu athari na madhara ya matumizii ya dawa za kulevya kwa ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

“Tunawahimiza kuacha kujihusisha na shughuli zinazokinzana na sheria, taratibu na kanuni za nchi yetu badala yake vijana tutumie mazingira wezeshi tuliyowekewa na Serikali kuongeza ufanisi katika kukuza taaluma, uchumi, elimu na biashara ili kufikia malengo yetu hivyo napenda kuwahakikishia kuwa Ofisi ya Mkuuwa Wilaya tutaendelea kushirikiana na wadau wote wa vijana kwa kuwawekea mazingira rafiki ili muweze kutekeleza majukumu yenu ipasavyo.” Amesisitiza Mhe. Mpogolo

Katika hatua nyingine Mhe. Mpogolo amewasihi vijana na wananchi wa Wilaya ya Ilala kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Octoba 2024 huku akiwataka kujitokeza kwa wingi katika kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura pindi litakapofunguliwa.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam Mhe. Omary Kumbilamoto ameeleza kuwa ni mpango wa Serikali sasa katika kuhakikisha waraibu wote wa matumizi ya dawa za kulevya wanapewa huduma ya matibabu kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ambapo kwa sasa Serikali inaboresha kwanza huduma za afya kisha waanze kuratibu mpango huo hivyo amewasihi vijana wa Vingunguti kuhakikisha wana nitoke za kwa wingi kupata tiba na elimu.

Awali akisoma taarifa kwa Mkuu wa Wilaya Mratibu wa Shirika la utoaji elimu juu ya matumizi ya dawa za kulevya (NURGET) Bw.John Samson Busumabu ameeleza kuwa Taarifa ya Dawa za kulevya duniani inaonesha kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la biashara na matumizi ya Dawa za kulevya ambapo hali ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2021 ilionesha kuwa, takribani mtu 1 kati ya kila watu 17 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 ulimwenguni walitumia Dawa za Kulevya. Katika kipindi cha mwaka uliopita, Idadi iliyokadiriwa ya watumiaji wa Dawa za Kulevya kwa miaka kumi imeongezeka kutoka milioni 240 mwaka 2011 hadi milioni 296 mwaka 2021 ambalo ni ongezeko la asilimia 23%. ambapo Katika kipindi hicho, Dawa za kulevya kama bangi, heroin, metamphetamine, cocaine pamoja na Dawa tiba zenye asili ya kulevya zilitumika. Mwaka 2020, inakadiriwa kuwa watu milioni 36 walitumia Dawa za kulevya jamii ya amphetamine (ATS), milioni 22 walitumia cocaine, na milioni 20 walitumia dawa aina ya “ecstasy” zilizopelekea madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii, kama vile ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya akili na homa ya ini hivyo, jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti uzalishaji, biashara na matumizi ya Dawa za Kulevya, ikiwa ni pamoja na utoaji wa tiba kwa watu wenye uraibu wa dawa hizo.

Aidha Bw. Busumabu ameeleza kuwa Halmashuri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kuungana na Wananchi wote Nchini na Duniani kote katika harakati za kudhibiti na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya kwani Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam itaendelea kutoa elimu juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya ili kuzuia na kukinga watoto na vijana ambao hawajaingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya na kuhakikisha kuwa hawaingii kwenye matumizi hayo huku wakiendelea kusaidiana na Serikali kupitia Mamlaka husika kuhakikisha linazuia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa Dawa za kulevya nchini ili kuinusuru jamii dhidi ya Dawa za kulevya bila kusahau kuwatambua waraibu wa Dawa za kulevya na kuwaelimisha juu ya huduma za upunguzaji madhara ili kuchangia katika kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya kwa kuwaunganisha na huduma za afya kama kuwapeleka MAT kliniki kwa ajili ya kupata dawa ya maethadone ikiwa ni pamoja na kupata tiba za TB, Homa ya Ini na kupata dawa za ARV kwa walio na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Katika Kongamano hilo mada mbalimbali ziliweza kutolewa kwa vijana wapatao 1000 walioshiriki ikiwemo Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya ,Haki na Wajibu wa Kijana Kipindi cha Uchaguzi, Fursa za Kiuchumi kwa Vijana, Faida na Hasara ya mitandao ya Kidigitali, jinsi ya kujikinga na maambukizi dhidi ya VVU/ UKIMWI pamoja na namna ya kuwa wazalendo na kujitolea kwa Vijana.

# Shilingi bilioni 10.75 kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa Barabara Jiji la DSM



Shilingi bilioni 10.75 fedha kutoka mapato ya Halmashauri zimetengwa kwaajili ya ujenzi wa barabara Jijinla Dar es Salaam kwa kiwango cha lami.

Hayo yamebainishwa Julai 15,2024, na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam Ndugu Jomaary Satura kwenye hafla fupi ya utiaji saini mikataba ya ujenzi wa barabara 10 kati ya Jiji la Dar es Salaam na wakandarasi wanaoenda kutekeleza miradi hiyo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo amewataka Wakandarasi kuwa waadilifu kwa kuhakikisha wanakamilisha miradi kwa wakati huku akiwasisitiza washirikiane katika kazi ili kuleta matokeo yenye tija kwa maslahi ya Wananchi.

Sambamba na hilo Mhe. ametoa pongezi kwa Mstahiki Meya na Madiwani kwa usimamizi mzuri wa miradi huku akimpongeza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na watendaji wa Jiji kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato ambao umekua chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam Mhe.Omary Kumbilamoto amemshukuru Rais Wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa fedha anazotoa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo huku akitoa wito kwa Wakandarasi kutekeleza miradi kwa wakati uliopangwa ilo waweze kutimiza adhma ya Rais ya kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi kwa wakati.

Awali akizungumza wakati wa hafla hiyo Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam Ndug. Jomaary Satura ameeleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imejipanga kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi kwa kuzingatia nyanja zote muhimu ikiwemo elimu, afya na miundombinu hivyo katika kutekeleza hilo JiJi la Dar es Salaam limeweza kutenga asilimia 10 za mapato ya ndani kwaajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara ambapo bilioni 10.7 itatumika kutekeleza miradi hiyo

“Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tumekusanya shilingi bilioni 111 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 sawa na ongezeko la bilioni 30 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023 hivyo kutokana na mapato haya kuongezeka shilingi bilioni 10.7 imetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara 10 za ndani Jiji la Dar es Salaam zinazoenda kutekelezwa kwa kiwango cha lami na zege na leo tunasaini mikataba na wakandarasi wanaoenda kutekeleza miradi hiyo, hivyo niimani yangu wakandarasi waliochaguliwa ni wakandarasi wenye uwezo wa kujisimamia wenyewe na watakamilisha mradi kwa wakati pia niwatake muwe waadilifu kwa kutekeleza majukumu ipasavyo kwa faida ya watanzania wengine.”Amesisitiza Ndug. Satura

Naye Mkandarasi kutoka Kampuni ya Southern Link Bw. John Mosha ameishukuru Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kuchaguwa wakandarasi wazawa huku akiwahakikishia kutekeleza miradi hiyo kwa kiwango bora na kwa wakati.

Aidha Miradi hii inatarajiwa kukamilika ndani ya muda wa miezi mitatu..



# Vioongozi na Watendaji wa Halmashauri ya Rungwe, wafanya ziara Halmashauri ya Jiji DSM



Viongozi na watendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Rungwe wamefanya ziara ya mafunzo katika Halmshauri ya jiji la DSM

Jiji la Dar es Salaam, tarehe 08 Julai, 2024, limepokea ujumbe wa viongozi , na Watendaji wapatao 54 kutoka katika Halmashauri ya wilaya ya Rungwe iliyopo mkoani Mbeya, waliofanya ziara ya kujifunza mbinu mbali mbali za ukusanyaji wa mapato, usafi wa mazingira na Usimamizi na wa miradi. Katika Ziara hii wametembelea soko la samaki feri.



Ujumbe huo uliongozwa na Mkuu wa wilaya Rungwe Mh. Jafari Haniu ambaye amewashukuru viongozi na watendaji wa jiji la dar es salaam kwa kukubali kuwapatia mafunzo hayo.pia amewapongeza kwa jiji bora katika ukusanyaji wa mapato.

Akiongea wakati wa kufungua mafunzo hayo yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Arnatoglou, Naibu Meya wa Jiji la Dar es Salaam Didas Odjambi amesema “Nachukua nafasi hii kuwakaribisha katika Jiji la Dar es Salaam na tumefarijika kupokea ugeni huu mkubwa kutoka Rungwe hii inatupa uwezo wa kubadilishana uzoefu, sisi tuwape yetu lakini pia tupokee kutoka kwenu.”

Mwanyekiti wa kamati ya Halmashauri ya wilaya ya Rungwe Mhe. Mpokigwa Mwankuga amesema kuwa wamejifunza mambo mengi mazuri ambayo hapo awali walikuwa hawayafahamu hivyo kwa namna moja au nyingine yatabadilisha utendaji wao wa kazi na kuleta matokeo chanya katika Halmashauri yao.



“Tumejifunza mambo mengi ambayo tulikuwa hatuyafahamu hapo awali. Tumejifunza mbinu hasa uanzishwaji wa kanda katika kusimamia na kukusanya mapato na usafi wa mazingira . Nina imani haya yote tuliyojifunza tukiyaweka kwenye utekelezaji tutakuwa tumepiga hatua kubwa.”

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa ikipokea wageni mara kwa mara kutoka ndani na nje ya nchi wanaokuja kujifunza namna inavyotekeleza majukumu yake na kupata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kama ukusanyaji mapato.

# Kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa, Jiji la DSM lafanya Usafi wa Mazingira maeneo ya Feri



Katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya Mashujaa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Kitengo cha udhibiti wa taka na usafi wa mazingira kwa kushirikiana na Kitengo cha maliasili na uhifadhi wa Mazingira Julai 24, 2024 wamefanya usafi wa mazingira katika eneo la Soko la Kimataifa la Samaki Feri na Stendi ya Kivukoni ikiwa ni sehemu ya kuwaenzi mashujaa waliopoteza maisha yao katika kutetea na kulinda Uhuru wa Tanzania.

Akizungumza katika zoezi hilo Mkuu wa Kitengo cha udhibiti wa taka na usafi wa Mazingira Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bw. Rajabu Ngoda ameeleza kuwa **"Katika kuelekea Kilsisi kama Halmashauri ya Jiji tumewakumbuka mashujaa wetu kwa kufanya usafi katika maeneo haya ya Kivukoni hivyo niwahimize Wananchi, wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa mazingira kuhakikisha mnafanya usafi wa kila siku katika maeneo bila kushurutishwa lengo likiwa ni kuweka mazingira ya Jiji la Dar es Salaam katika hali ya usafi lakini pia kuepuka na magonjwa ya mlipuko".**

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na uhifadhi wa Mazingira Jiji la Dar es Salaam Bi. Theresia Denis ameeleza kuwa mbali na kuwakumbuka Mashujaa waliopigania Uhuru pia usafi huo umekua ni sehemu ya kuwakumbusha Wananchi kutunza mazingira ya Jiji kwa ajili ya afya ya Jamii huku akiwahimiza kufanya usafi kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku na sio kusubiri matukio maalumu.

Naye Meneja wa Soko la Kimataifa la Samaki Feri ametoa wito kwa Wafanyabiashara wa Soko hilo kuhakikisha wanatunza mazingira kwa kuyaweka katika hali ya usafi kabla na baada ya kumaliza biashara zao.

Aidha Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa huadhimishwa kila tarehe 25 Julai ya kila Mwaka.





HALMASHAURI YA JIJI
LA DAR ES SALAAM

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wamiliki wote wa Majengo kuwa

# ZOEZI LA UKUSANYAJI TAARIFA ZA KODI YA MAJENGO

**litaanza Tarehe 22, Julai 2024**

Hivyo kila mmiliki wa Jengo anapaswa kuandaa Taarifa muhimu ili kufanikisha Zoezi hilo ikiwemo

- Kitambulisho cha NIDA / NAMBA
- Namba ya Mita ya LUKU
- Block na Plot namba au Post Code
- Kwa nyumba zinazomilikwa na Makampuni wawe na TIN Namba
- Kwa nyumba zinazomilikwa na Mtu zaidi ya mmoja yaani ( Condonimum ) kuwe na taarifa za kila mmiliki

Zoezi hili litasimamiwa na Viongozi wa Serikali ya Mtaa wako, hivyo kila Mwananchi anaombwa kutoa ushirikiano

Tangazo hili limetolewa na :
Mkurugenzi wa Jiji la DSM

jiji_la_dsm
www.dcc.go.tz